**UGANDA MARTYRS UNIVERSITY**

**DEPARTMENT OF KISWAHILI, 2024**

**SEMISTER TWO EXAMS**

**YEAR ONE**

**BACHELOR OF EDUCATION PRIMARY**

**KLE 61202: KISWAHILI LANGUAGE SKILLS**

**DURATION: 3HRS**

## MAAGIZO

- Jibu maswali manne kwa yote .
- Kila swali liandiiwe kwa ukurasa mpya wa karatasi ya majibu.
- Usiandike kokote kwenye karatasi ya maswali.
- 

1. (a) Taja na ufafanue stadi nne za lugha ya Kiswahili

(b). Fafanua jinsi unaweza kufundisha stadi hizi za lugha kwa wanafunzi wako wa darasa la nne.

i. Kusikiliza
ii. Kusema
iii. Kusoma
iv. Kuandika

2. (a) Eleza sifa za insha bora.

(b). Fafanua jinsi unavyoweza kufundisha stadi ya kusikiliza katika darasa la sita.

© Uganda Martyrs University,2024.

3. (a) Chagua mada Moja kutoka miongoni mwa zilizoko hapa chini kisha utunge insha yenye maneno kati ya (150-250).

(i) Andika hotuba yako ambayo utatoa mbele ya wapigaji kura wako baada kushinda kiti cha ubunge wilayani mwako

(ii) Andika ripoti Kwa afisa wa polisi ya babarani kuhusu kisa Cha ajali ya basi iliyotokea kwenye mji wa Kayabwe.

(iii) Andaa kumbukumbu za mkutano wa chama cha ukuzaji wa Kiswahili katika chuo chenu kuhusu mipango na mikakati ya kuendeleza Kiswahili chuoni mwenu.

4 .(a) Eleza sifa za insha bora.(Alama 12)

(b). Fafanua jinsi unaweza kufundisha stadi ya kusikiliza katika darasa la sita.(Alama 13).

5. (a). Fafanua maana na dhana ya mawasiliano (Alama 07).

(b).Eleza mambo Sita ambayo yanaweza kutatiza mawasiliano baina ya watu wawili. (Alama 18).

6. Akifisha hadithi hii ifaavyo.

hapo zamani za kale paliishi mbuni na mamba. wanyama hawa walipendana chanda na pete Cha mbuni kilikuwa cha mamba Kila uchapo mbuni alienda kuwinda na angebahatika kupata chakula bila shaka angefululiza moja kwa moja na kuenda mpatia rafiki yake mambo aliyeishi majini, vivyo hivyo mamba naye aliposhika mnyama kule majini angeweka kipande kikubwa Kwa rafikiye mbuni. Urafiki wao ulidumu Kwa muda.

Maajabu na majaribu yalitokea wakati ambapo siku moja ilikuwa yenye mkosi ambapo mbuni aliwinda siku njema lakini kubahatika kunasa hata nzi, naye mamba kule majini licha ya kutumia mbinu zote na nguvu ili apate windo jitihada zake hazikufua dafu. Ilionekana kuwa siku hii ilikuwa ya mama kumla mtotowe na ng'ombe kula kondo.

Njaa ilizidi kuvunja mifupa mamba akahisi main yanamchoma kama tanuri ya matofali, taya zake mamba zikaanza kumtetemeka na kiwiliwili chake kikawa baridi kama barafu. Ah nifanye nini, alijiuliza mamba. Nitakufa leo hii kabisa, sijawahi kuona njaa kama hii, aliongezea moyoni. Mwishoni shetani alimjia mamba akawa na wazo aliloliona kumfaa katika kipindi hiki Cha mateso ya njaa. Mbuni, mbuni rafiki yangu akijitokezea bila chakula Cha kunitosha bila shaka nitamla leo, nakufa leo nisipokula, mbuni.......! alisema moyoni huku akitoka majini kuelekea pakavu kumngoja mbuni.

Mbuni naye alipoona ameshindwa kabisa kupata windo aliona heri aende Kwa rafiki ambaye huenda keshapata kitu wagawane aweze kupona njaa iliyomvunja mifupa na koo mkauka. Leo

© Uganda Martyrs University,2024. 

ni siku ya balaa, njaa hii jamani Ina nini, alijisemea. Lakini kweli mamba ana kitu sifi njaa ikiwa yupo..... akazidi kujisemea huku akikaribia mahali pa mamba.

Mamba alimuona rafiki yake alija bila alichobeba kama kawaida yake. Hasira za njaa na mawazo ya kishetani yalizidi kumvamia Kwa haraka na kumparamia ubongoni. Najilaza hapa mchangani, sifi njaa mimi. Akajiambia.

Rafiki yangu mamba, njoo unione hapa, Mimi ni mgonjwa tangu Jana, jino oa gego laniuma na sijui karibu na kufa nakuacha rafiki yangu mpendwa. Akasema Kwa kuupole na huzuni nyingi.

Mbuni aliona kweli rafiki yake ni mgonjwa naye akamuomba aachame apanue kunywa chake amuone mdomoni kubaini kilichomuuma kinywani. Mamba alipanua kinywa chake Kwa Hila na kumwabia mbuni kuingiza kichwa chake na kubaini kilichomuuma.

Mbuni alipokiingiza kichwa chake mdomoni mwa mamba alipigwa na butwaa, akastanabahi na kugutuka alipoona mamba Kwa Kasi kama ya mtego amemshika na kumkaba mle kinywani. Mbuni akijaribu kupiga kelele kumuita rafikiye eti amemshika na kumpoteza hewa kinywani lakini aliona mamba anazidi kumkaba Koo na kumburuta akielekea majini. Hapo mbuni alijua kuwa mambo ni mabaya Sasa anahitaji Mungu kumnusuru huku naye akipigana kishujaa. Mbuni alijitupa huku na huku akapiga makofi mawili kwenye taya za mamba na huku akivuta shingo yake Kwa nguvu kujitoa kinywani mwa mamba aliyeelekea kufupisha maisha yeke Kwa sekunde Moja hiyo. Bahati nzuri mbuni alifanukiwa kujitoa kinywani mwa mamba lakini shingo yake ilireefuka na hadi Sasa umuonapo imereefuka.

7. (a) Tumia viakifishaji vifaavyo katika sentensi hizi.

i. Jana ilikuwa siku ya alhamisi, mwalimu aliwaambia Wanafunzi wake.
ii. Lo sijawahi kuona mtu kama wewe, alisema Kwa hasira
iii. Kumbe wewe una miaka mingapi ndipo uanze kuniulizauliza. Mzee aliuliza kijana
iv. Kama unataka kifo cha haraka songa mbele yangu nikuonyeshe. Askari mkali akasema.
v. edward njoo hapa tafadhali, akamuita Kwa hasira.
vi. ziwa la victoria ni kubwa kuliko la nyasa.
vii. mbunge wetu kabanda amejenga hospitali kubwa.
viii. askofu ni kiongozi wa dhehebu ya kikristo
ix. hapa pake au ni pako. (Alama 25).
x.

**MWISHO**

© Uganda Martyrs University,2024.